TANGAZO LA SERIKALI NA. 111 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MTAKUJA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mtakuja ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

*Tangazo la Serikali na. 111(linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba A yenye majira - nukta 450452.12MS, 9580316.01KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS $68^0$ 01'43.67"MS kwa umbali wa kilometa 2.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira – nukta 452544.14MS, 9579472.05KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS $32^0$ 09'47.55"MS kwa umbali wa kilometa 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba C yenye majira- nukta 453220.52MS, 9578397.11KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS$47^0$ 39'43.03"MG wa umbali wa kilometa 0.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira- nukta 452556.05MS, 9577792.21KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS$10^0$ 24'51.90"MS kwa umbali wa kilometa 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 452463.35MS, 9577286.71KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ$58^0$ 24'53.60"MG kwa umbali wa kilometa 0.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira – nukta 451749.12MS, 9577725.26KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ$21^0$ 40'58.82"MG kwa umabali wa kilometa 1 hadi kwenye alama ya mpaka ya uimaji namba G yenye majira – nukta 451417.21MS,9578560.31KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ$58^0$ 01'43.21.8"MG kwa umbali wa kilometa 1.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira - nukta 450134.26MS, 9579361.91KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ$68^0$ 01' 43 67"Mg kwa umbali wa kilometa hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*